# TOLEO LA TAKWIMU ZA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA KIJINSIA KWA WANAWAKE NA WATOTO -ZANZIBAR, JANUARI MWAKA 2022

**Na: 01**

*Office of Chief Government Statistician*

*P.O. Box 2321, Zanzibar*
Telephone +255242231869
Email: zanstat@ocgs.go.com
Website: http://www.ocgs.go.tz

*UN Women Office*
392Toure Drive, Masaki
Dar es Salaam
Tanzania

*Police Headquarter Zanzibar*

P.O.Box 237, PHQ Zanzibar
Fax No: 0242231367
Email:cidhqznz@gmail.com

## Utangulizi

Ofisi ya Mtakwimu Mkuu kwa kushirikiana na Shirika la Wanawake la Umoja wa Mataifa wameandaa utaratibu ambao utawezesha ofisi kutekeleza majukumu yake iliyojipangia kuimarisha takwimu za jinsia. Miongoni mwa takwimu hizo ni kukusanya takwimu za matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia.

Toleo hili hutolewa kila mwezi ambalo hutoa muhtasari wa takwimu za maeneo mawili ya uhalifu ambazo ni ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizi zinatolewa kwa kutofautiana kwa kijiografia, kimakundi na kjinsia.

Takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia hutoa taarifa za idadi ya matukio yaliyotokea, aina ya waathirika na hali ya waathirika baada ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia. Takwimu hizo hutoa taarifa kuhusu matukio ambayo yameainishwa katika makundi makuu sita (6).


## Lengo

Lengo kuu la kutolewa toleo hili ni kutoa taarifa za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia za ndani ya Zanzibar. Taarifa hizi ni muhimu na hutumiwa na wapangaji, watunga sera, na watoa maamuzi.

## Matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia

Jumla ya matukio 65 ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia yameripotiwa mwezi wa Januari, 2022. Kulikuwa na waathirika 65 ambao waathirika Wanawake ni16 (asilimia 24.6) na watoto ni 49 sawa na asilimia 75.4, miongoni mwao wasichana ni 43 (asilimia 87.8) na wavulana ni 6 (asilimia 12.2).


**Kielelezo 1.1: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto, Januari 2022**




**Chanzo: Makao** makuu ya Polisi –Zanzibar

Wilaya ya  Magharibi "B" imeripotiwa kuwa na matukio mengi ukilinganisha na wilaya nyengine (matukio 13), zikifuatia wilaya ya Wete (matukio 11) na wilaya ya Magharibi "A" (matukio 10). Wilaya ya Kaskazini "B" imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio kuliko wilaya zote (tukio moja (1)) ambapo wilaya ya Mkoani hakuna tukio lililoripotiwa.

**Kielelezo 1.2: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto kwa Wilaya, Januari 2022**




**Chanzo:** Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Mlinganisho wa idadi ya matukio kwa mwezi imepungua kwa asilimia 13.0 kutoka matukio 97 kwa mwezi wa December, 2021 hadi 65 mwezi wa Januari, 2022. Aidha wilaya Magharibi “B” iliongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa mwezi Disemba 2021 (matukio 20) na Januari 2022 (matukio 13). Wilaya ya Kaskazini “A” imeripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio kwa mwezi wa Disemba 2021 (matukio mawili (2)) ambapo wilaya ya Kaskazini “B” iliripotiwa kuwa na idadi ndogo ya matukio kwa mwezi wa Januari 2022 (tukio moja (1)) na wilaya ya Mkoani hakuna tukio lililoripotiwa kwa mwezi huu.

**Jadweli 1.1: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Mwezi Disemba 2021 na Januari 2022**

| Wilaya | Idadi ya matukio | | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Disemba 2021 | Januari 2022 | Disemba 2021 | Januari 2022 | Disemba 2021 | Januari 2022 | Disemba 2021 | Januari 2022 | Disemba 2021 | Januari 2022 | Disemba 2021 | Januari 2022 | Disemba 2021 | Januari 2022 |
| Kaskazini 'A' | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 9 | 1 | 6 | 1 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Kati | 5 | 6 | 5 | 3 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 3 | 3 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Mjini | 11 | 7 | 5 | 5 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 2 | 2 |
| Magharibi 'A' | 9 | 10 | 4 | 7 | 2 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 2 |
| Magharibi 'B' | 20 | 13 | 3 | 1 | 6 | 0 | 3 | 2 | 0 | 1 | 2 | 1 | 6 | 8 |
| Wete | 17 | 11 | 9 | 1 | 3 | 0 | 0 | 0 | 3 | 3 | 2 | 2 | 0 | 5 |
| Micheweni | 10 | 9 | 9 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 3 |
| Chake | 6 | 3 | 5 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 | 0 | 0 |
| Mkoani | 5 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **97** | **65** | **53** | **25** | **14** | **1** | **8** | **7** | **4** | **5** | **7** | **7** | **11** | **20** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Mlinganisho wa idadi ya matukio kwa mwaka imepungua kwa asilimia 46.7 kutoka matukio 122 kwa mwezi wa Januari, 2021 hadi 65 mwezi wa Januari, 2022. Wilaya ya Magharibi "A" iliongoza kwa idadi kubwa ya matukio kwa mwezi Januari, 2021 (matukio 28) ambapo wilaya ya Magharibi "B" iliongoza kwa mwezi wa Januari, 2022 (matukio 13).

**Jadweli 1.2: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Mwezi Januari 2021 na Januari 2022**

| Wilaya | Idadi ya matukio | | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | Januari 2021 | Januari 2022 | Januari 2021 | Januari 2022 | Januari 2021 | Januari 2022 | Januari 2021 | Januari 2022 | Januari 2021 | Januari 2022 | Januari 2021 | Januari 2022 | Januari 2021 | Januari 2022 |
| Kaskazini 'A' | 16 | 2 | 12 | 0 | 3 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 12 | 1 | 8 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 |
| Kati | 6 | 6 | 4 | 3 | 0 | 1 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 3 | 3 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 0 |
| Mjini | 18 | 7 | 5 | 5 | 4 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 6 | 2 |
| Magharibi 'A' | 28 | 10 | 11 | 7 | 9 | 0 | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 5 | 2 |
| Magharibi 'B' | 13 | 13 | 6 | 1 | 1 | 0 | 2 | 2 | 0 | 1 | 0 | 1 | 4 | 8 |
| Wete | 4 | 11 | 3 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 1 | 2 | 0 | 5 |
| Micheweni | 5 | 9 | 5 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 | 2 | 0 | 3 |
| Chake Chake | 9 | 3 | 3 | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 2 | 1 | 0 | 0 |
| Mkoani | 8 | 0 | 4 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **122** | **65** | **61** | **25** | **22** | **1** | **6** | **7** | **9** | **5** | **7** | **7** | **17** | **20** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Miongoni mwa waathirika wa ukatili na udhalilishaji wa kijinsia waliobakwa ni 25, wanawake walikuwa wawili (2) na wasichana ni 23, aliolawitiwa ni mmoja(1), Kuingiliwa kinyume na maumbile saba(7)(mwanamke alikuwa mmoja (1) na wasichana ni sita (6)), Kutorosha walikuwa watano (5) wote ni wasichana, shambulio la aibu walikuwa saba (7) (wanawake watatu (3) na wasichana walikuwa wanne (4)) na shambulio walikuwa 20 (wanawake ni 10, wasichana watano (5) na wavulana walikuwa watano (5)).

**Jadweli 1.3: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Januari 2022**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | |
| | | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana |
| Kaskazini 'A' | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 6 | 3 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mjini | 7 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Magharibi 'A' | 8 | 6 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 1 |
| Magharibi 'B' | 11 | 1 | 0 | 2 | 1 | 0 | 1 | 0 | 3 | 3 |
| Wete | 6 | 1 | 0 | 0 | 3 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Micheweni | 4 | 2 | 0 | 0 | 1 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Chake Chake | 2 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **49** | **23** | **1** | **6** | **5** | **0** | **4** | **0** | **5** | **5** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

**Jadweli 1.4: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake kwa Wilaya, Januari 2022**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mjini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'A' | 2 | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 |
| Magharibi 'B' | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Wete | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 |
| Micheweni | 5 | 1 | 0 | 0 | 1 | 3 |
| Chakechake | 1 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **16** | **2** | **1** | **0** | **3** | **10** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Watoto wenye umri wa miaka 15-17 wameripotiwa kuwa na idadi kubwa ya matukio (matukio 22) sawa na asilimia 44.9 ya matukio yote ya watoto yalioripotiwa ikifuatiwa na umri wa miaka 11-14 (matukio 15) sawa na asilimia 30.6. Aidha matukio ya kubaka yanaonesha kuwa mengi zaidi katika umri wa miaka 15-17(matukio 12).

**Jadweli 1.5: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Januari 2022**

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | |
| | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | Wavulana | Wasichana | |
| 0-5 | | 2 | 0 | | | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 5 |
| 6-10 | | 3 | 1 | | | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 7 |
| 11-14 | | 6 | 0 | | | 2 | 0 | 4 | 0 | 0 | 1 | 2 | 15 |
| 15-17 | | 12 | 0 | | | 1 | 0 | 1 | 0 | 1 | 4 | 3 | 22 |
| **Jumla** | | **23** | **1** | | | **6** | **0** | **5** | **0** | **4** | **5** | **5** | **49** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Idadi ya watoto waathirika wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa mwezi wa Januari, 2022 imepungua kwa asilimia 45.6 (matukio 49) ukilinganisha na mwezi wa Disemba, 2021 (matukio 90). Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika wenye umri wa miaka 15-17 kwa mwezi uliopita imepungua kwa asilimia 56.0 kutoka matukio 50 kwa mwezi Disemba 2021 hadi matukio 22 kwa mwezi wa Januari 2022.

**Jadweli 1.6: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Mwezi Disemba 2021 na Januari 2022**

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Disemba 2021 | Jumla Januari 2022 |
| | Disemba 2021 | Januari 2022 | Disemba 2021 | Januari 2022 | Disemba 2021 | Januari 2022 | Disemba 2021 | Januari 2022 | Disemba 2021 | Januari 2022 | Disemba 2021 | Januari 2022 | | |
| 0-5 | 1 | 2 | 3 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 3 | 0 | 0 | 5 | 5 |
| 6-10 | 5 | 3 | 2 | 1 | 1 | 3 | 0 | 0 | 2 | 0 | 1 | 0 | 11 | 7 |
| 11-14 | 11 | 6 | 6 | 0 | 4 | 2 | 1 | 4 | 1 | 0 | 1 | 3 | 24 | 15 |
| 15-17 | 36 | 12 | 3 | 0 | 2 | 1 | 3 | 1 | 1 | 1 | 5 | 7 | 50 | 22 |
| **Jumla** | **53** | **23** | **14** | **1** | **7** | **6** | **4** | **5** | **5** | **4** | **7** | **10** | **90** | **49** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Mlinganisho wa idadi ya watoto waathirika wenye umri wa miaka 15-17 kwa mwaka uliopita imepungua kwa asilimia 52.0 kutoka matukio 102 kwa mwezi wa Januari, 2021 hadi matukio 49 kwa mwezi wa Januari, 2022. Hata hivyo, umri huu umeonyesha kuwa na waathirika wengi zaidi kuliko umri mwengine na umri wa 0-5 ulikuwa na waathirika kidogo kwa miezi hiyo.


**Jadweli 1.7: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Watoto kwa Wilaya, Mwezi Januari 2021 na Januari 2022**

| Miaka | Aina ya ukatili na udhalilishaji | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Januari 2021 | Jumla Januari 2022 |
| | Januari 2021 | Januari 2022 | Januari 2021 | Januari 2022 | Januari 2021 | Januari 2022 | Januari 2021 | Januari 2022 | Januari 2021 | Januari 2022 | Januari 2021 | Januari 2022 | | |
| 0-5 | 1 | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 | 0 | 3 | 0 | 0 | 3 | 5 |
| 6-10 | 0 | 3 | 8 | 1 | 2 | 3 | 1 | 0 | 2 | 0 | 3 | 0 | 16 | 7 |
| 11-14 | 12 | 6 | 10 | 0 | 1 | 2 | 1 | 4 | 1 | 0 | 5 | 3 | 30 | 15 |
| 15-17 | 38 | 12 | 4 | 0 | 1 | 1 | 5 | 1 | 1 | 1 | 4 | 7 | 53 | 22 |
| **Jumla** | **51** | **23** | **22** | **1** | **6** | **6** | **7** | **5** | **4** | **4** | **12** | **10** | **102** | **49** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Matukio 51 kati ya matukio 65 yanaonekana yametokea sehemu nyengine  sawa na asilimia 78.5 na  matukio 14 yametokea nyumbani sawa na asilimia 21.5.

**Kielelezo 1.3: Idadi ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto na Sehemu Yaliyotokea, Januari 2022**




Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Mlinganisho wa matukio yaliyotokezea nyumbani kwa mwezi yamepungua kwa asilimia 82.5 kutoka matukio 80 kwa mwezi wa Disemba, 2021 hadi matukio  14 kwa mwezi wa Januari, 2022, ambapo matukio yaliyotokea sehemu nyengine yameongezeka kwa kiasi kikubwa  kwa mwezi wa Januari 2022.

**Jadweli 1.8: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto na Maeneo yaliyofanyika Matukio, Disemba 2021 na Januari 2022**

| Eneo la matukio | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Disemba 2021 | Jumla Januari 2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Disemba 2021 | Januari 2022 | Disemba 2021 | Januari 2022 | Disemba 2021 | Januari 2022 | Disemba 2021 | Januari 2022 | Disemba 2021 | Januari 2022 | Disemba 2021 | Januari 2022 | | |
| Nyumbani | 39 | 3 | 13 | 1 | 7 | 2 | 4 | 1 | 6 | 2 | 11 | 5 | 80 | 14 |
| Kazini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli/Madrasa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu nyengine | 14 | 22 | 1 | 0 | 1 | 5 | 0 | 4 | 1 | 5 | 0 | 15 | 17 | 51 |
| **Jumla** | **53** | **25** | **14** | **1** | **8** | **7** | **4** | **5** | **7** | **7** | **11** | **20** | **97** | **65** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Mlinganisho wa idadi ya matukio yaliyotokea nyumbani kwa mwaka uliopita imepungua kwa asilimia 85.1 kutoka matukio 94 kwa mwezi wa Januari, 2021 hadi 14 mwezi wa Januari, 2022 ambapo matukio yaliyotokea sehemu nyengine yameongezeka kwa asilimia 82.1 kutoka matukio 28 kwa mwezi wa Januari 2021 hadi matukio 51 kwa mwezi wa Januari 2022.

**Jadweli 1.9: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto na Maeneo yaliyofanyika Matukio, Januari 2021 na Januari 2022**

| Eneo la matukio | Kubaka | | Kulawiti | | Kuingilia kinyume na maumbile | | Kutorosha | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | Shambulio | | Jumla Januari 2021 | Jumla Januari 2022 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Januari 2021 | Januari 2022 | Januari 2021 | Januari 2022 | Januari 2021 | Januari 2022 | Januari 2021 | Januari 2022 | Januari 2021 | Januari 2022 | Januari 2021 | Januari 2022 | | |
| Nyumbani | 47 | 3 | 16 | 1 | 5 | 2 | 5 | 1 | 4 | 2 | 17 | 5 | 94 | 14 |
| Kazini | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli/Madrasa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu nyengine | 14 | 22 | 6 | 0 | 1 | 5 | 4 | 4 | 3 | 5 | 0 | 15 | 28 | 51 |
| **Jumla** | **61** | **25** | **22** | **1** | **6** | **7** | **9** | **5** | **7** | **7** | **17** | **20** | **122** | **65** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

Matukio 54 kati ya matukio 65 yaliyoripotiwa yapo chini ya upelelezi wa Polisi na matukio 11 yapo hatua nyengine (ambapo matukio sita (6) yapo Ofisi ya Mashtaka na matukio matano (5) yapo mahakamani.


**Jadweli 1.10: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto na Hatua Zilizochukuliwa, Januari 2022**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | Waathirika | | | Hatua zilizochukuliwa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Wanawake | Watoto | | Zilizo Mahakamani | Zilizotiwa hatiani | Ziliachiwahuru | Zilizofungwa Polisi | Zilizopelekwa kwa Ofisi ya M' mashtaka | Zilizo chini ya Upelelezi wa Polisi |
| | | | Wasichana | Wavulana | | | | | | |
| Kubaka | 25 | 2 | 23 | | 3 | 0 | 0 | 0 | 4 | 18 |
| Kulawiti | 1 | | | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 7 | 1 | 6 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 | 5 |
| Kutorosha | 5 | 0 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 7 | 3 | 4 | 0 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 6 |
| Shambulio | 20 | 10 | 5 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 20 |
| **Jumla** | **65** | **16** | **43** | **6** | **5** | **0** | **0** | **0** | **6** | **54** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi -Zanzibar

Wafanyaji wa matukio ya ukatili na udhalilishaji wa Kijinsia walioripotiwa kwa mwezi wa Januari 2022 ni 65 wote walikuwa wapita njia  sawa na asilimia 100.

**Kielelezo 1.4: Aina ya Watu Waliofanya Matukio ya Ukatiki na Udhalilishaji wa Kijinsia, Januari 2022**




Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

## Kiambatanisho

**Jadweli 1.0: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto na Maeneo yaliyofanyika Matukio, Januari 2022**

| Eneo la matukio | Kubaka | | | Kulawiti | | | Kuingilia kinyume na maumbile | | | Kutorosha | | | Shambulio la aibu/Kukashifu | | | Shambulio | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla | W'ke | W'me | Jumla |
| Nyumbani | 3 | [redacted] | 3 | [redacted] | 1 | 1 | 2 | [redacted] | 2 | 1 | 0 | 1 | 2 | 0 | 2 | 4 | 1 | 5 |
| Kazini | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Skuli/Madrasa | 0 | [redacted] | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | [redacted] | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Sehemu nyengine | 22 | [redacted] | 22 | [redacted] | 0 | 0 | 5 | [redacted] | 5 | 4 | 0 | 4 | 5 | 0 | 5 | 11 | 4 | 15 |
| **Jumla** | **25** | [redacted] | **25** | [redacted] | **1** | **1** | **7** | [redacted] | **7** | **5** | **0** | **5** | **7** | **0** | **7** | **15** | **5** | **20** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

**Jadweli 2.0: Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wilaya, Januari 2022**

| Wilaya | Idadi ya matukio | Aina ya ukatili na udhalilishaji Zanzibar | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Kubaka | Kulawiti | Kuingilia kinyume na maumbile | Kutorosha | Shambulio la aibu/Kukashifu | Shambulio |
| Kaskazini 'A' | 2 | 0 | 0 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Kaskazini 'B' | 1 | 1 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Kati | 6 | 3 | 1 | 2 | 0 | 0 | 0 |
| Kusini | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mjini | 7 | 5 | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Magharibi 'A' | 10 | 7 | 0 | 1 | 0 | 0 | 2 |
| Magharibi 'B' | 13 | 1 | 0 | 2 | 1 | 1 | 8 |
| Wete | 11 | 1 | 0 | 0 | 3 | 2 | 5 |
| Micheweni | 9 | 3 | 0 | 0 | 1 | 2 | 3 |
| Chake Chake | 3 | 2 | 0 | 0 | 0 | 1 | 0 |
| Mkoani | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Jumla** | **65** | **25** | **1** | **7** | **5** | **7** | **20** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

**Jadweli 3.0: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto, Mwezi Disemba 2021 na Januari 2022**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | | Waathirika | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | |
| | Disemba 2021 | Januari 2022 | Disemba 2021 | Januari 2022 | Disemba 2021 | Januari 2022 | Disemba 2021 | Januari 2022 |
| Kubaka | 53 | 25 | 0 | 2 | 53 | 23 | | |
| Kulawiti | 14 | 1 | | | | | 14 | 1 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 8 | 7 | 1 | 1 | 7 | 6 | | |
| Kutorosha | 4 | 5 | 0 | 0 | 4 | 5 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 7 | 7 | 2 | 3 | 5 | 4 | 0 | 0 |
| Shambulio | 11 | 20 | 4 | 10 | 1 | 5 | 6 | 5 |
| **Jumla** | **97** | **65** | **7** | **16** | **70** | **43** | **20** | **6** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi -Zanzibar

**Jadweli 4.0: Mlinganisho wa Takwimu za Aina ya Matukio ya Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto, Mwezi Januari 2021 na Januari 2022**

| Aina ya matukio | Idadi ya matukio | | Waathirika | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Wanawake | | Watoto | | | |
| | | | | | Wasichana | | Wavulana | |
| | Januari 2021 | Januari 2022 | Januari 2021 | Januari 2022 | Januari 2021 | Januari 2022 | Januari 2021 | Januari 2022 |
| Kubaka | 61 | 25 | 10 | 2 | 51 | 23 | | |
| Kulawiti | 22 | 1 | | | | | 22 | 1 |
| Kuingiliwa kinyume na maumbile | 6 | 7 | 0 | 1 | 6 | 6 | | |
| Kutorosha | 9 | 5 | 2 | 0 | 7 | 5 | 0 | 0 |
| Shambulio la aibu/Kukashifu | 7 | 7 | 3 | 3 | 3 | 4 | 1 | 0 |
| Shambulio | 17 | 20 | 5 | 10 | 6 | 5 | 6 | 5 |
| **Jumla** | **122** | **65** | **20** | **16** | **73** | **43** | **29** | **6** |

Chanzo: Makao makuu ya Polisi –Zanzibar

**Zingatia Maelezo**

**Ukatili na Udhalilishaji wa Kijinsia**

Kitendo chochote au mwenendo wowote, ambao husababisha moja kwa moja kwa mtu, kama mateso ya kimwili, ya kimapenzi au ya kiakili kupitia vitisho, kulazimisha au njia zingine; lengo la kutisha, kuadhibu, kuwadhalilisha, kudhoofisha usalama au kujiheshimu; kutosheleza hamu ya ngono; au kudhoofisha uwezo wa mwili au kiakili wa mtu kwa sababu ya jinsi yake. Kwa mfano, unyanyasaji wa kijinsia, kumpiga mke, unyanyasaji wa kijinsia wa wasichana na wavulana, ukeketaji wa kike, mwanamke kuua watoto wachanga, utoaji mimba, ukahaba wa kulazimishwa , Biashara haramu ya usafirishaji wa wanawake na watoto wa kike na ponografia (uenezaji wa ngono haramu).

Sheria ya Adhabu ya 6/2018 iliongeza adhabu kwa makosa yanayohusiana na maadili kama vile ubakaji, kulawiti, kuingilia kinyume na kimaumbile na shambulio la aibu;

Sheria hii imetungwa mwaka 2018 ambayo imekuja kufuta sheria kama hii ya mwaka 2004. Sheria hii imetungwa pamoja na mambo mengine kuyafanya baadhi ya matendo kuwa makosa ya jinai na kuyawekea adhabu zake endapo mtu yeyote atayatenda matendo hayo na mahkama itamuona ana hatia. Kwenye shehemu ya kumi na tatu (Section thirteen) ya sheria ya adhabu imejumuisha makosa mengi ambayo ni makosa dhidi ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa wanawake na watoto

Sheria ya mwenendo wa Jinai 7/2018 kifungu cha 151 (1) kina vifungu ambavyo haviruhusu utoaji wa dhamana kwa mtu yeyote anayeshtakiwa kwa kesi zinazohusiana na ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, pamoja na kuongezeka kwa hukumu ambazo Mahakama zinaweza kupitisha. Kwa mfano, katika Mahakama ya Mkoa kesi za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kutoka miaka 7 hadi miaka 14 na kwa Mahakama Kuu kutoka miaka 30 hadi kifungo cha maisha.

**Kwa ufafanuzi zaidi tafadhali wasiliana na:**

***Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali***
***Sanduku la barua, 2321***
***Barua pepe: zanstat@ocgs.go.tz***

***Makao Makuu ya Polisi Zanzibar***
***Sanduku la barua, 237, MMP, Zanzibar***
***Barua pepe:cidphqznz@gmail.com***